



Maswali na majibu (PLWHA)

Q. PLWHA ina maanisha nini?

Hii ni jina ya kizungu na kwa kiswahili inamaanisha watu ambao wanaishai na ugonjwa wa ukimwi.

Q. Ni sawa kuwa karibu na PLWHA ?

Ndio! Ni sawa kufanya kazi ,kusoma,kuishi na kucheza na mtu mwenye virusi vya ukimwi. Pia ni sawa watoto wenye virusi na wale hawana kucheza pamoja, mtu hawezi pata virusi vya ukimwi kwakufanya vitu kama :kusalimiana ,kubusu,kuvaa nguo pamoja, kutumia choo moja,kunywa maji pamoja na vitu vingine.Virusi vya huambukizwa kwa kubadilishana majimaji ya mwili ya mwanamke,mwanamume, damu na maziwa ya mama. Kama mtu hajapatana na majimaji hizi basi hayuko katika hatari yoyote ya kupata virusi vya ukimwi.Watu wenye ndio walimu wazuri wa kufundisha juu ya ugonjwa wa ukimwi na pia husaidia watu wengine wenye viruis na hawawezi kujisaidia. Watu wenye virusi hawapaswi kudharauliwa na wanapaswa kupendwa na kuheshima.

Q. Naweza pata virusi vya ukimwi kwa njia gani?

Kuna njia tatu ya kupata viruis vya ukimwi :

kwanza kufanya mapenzi bila kutumia kinga na mtu mwenye virusi vya ukimwi.

Pili Ni kwa njia ya damu kwa damu.Damu ya mtu mwenye virusi kupatana na damu ya mtu mwenye hana virusi kwa mfano kidonda ,kutumia makali pamoja ama kuongezwa damu ambayo haijapimwa.

Tatu ni mama mwenye virusi kupitishia mtoto wake.

Q. Je damu aumajimaji ya mwili ikinimwagikia kwenye ngozi?

Hata majimaji yoyote yenye virusi ikikumwagikia kwenye ngozi haiwezi kukudhuru.

Ni lazima virusi iingie kwenye damu ili mtu aweze kuambukizwa ugonjwa huu.

Q. Napaswa kujichunga kwa njia gani?

Kuna njia ambazo unapaswa kufuata ili ujichunge kutokana na virusi hivi.Njia hizi zinatumika sana na watu wale ambao wana fanya kazi na watu wenye virusi vya ukimwi.Kwanza wakati wa kuosha majimaji ya mwili ama kuogesha mtu ni vizuri kuvaa glovu.Pia pale damu au majimaji ilikuwa inaaswa kuoshwa n asababu na kemikali.Pia wakati wakatupa vitu ambavyo vimetumiwa na mtu mwenye viruis vya ukimwi wanapaswa kuziweka kwa karatasi ya plastiki na kuzifunga kwa uhakika, pia baada ya kutoa glovu ni muhimu kuosha mkono na sabuni.